# TUKIJUA HILI KWAMBA UTU WETU WA KALE UMESULUBISHWA PAMOJA NAYE

*……" Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; tukijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulubishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena"* (Warumi 6:5-6).
…. Lakini mimi, hasha, nisione fahari juu ya kitu chochote ila msalaba wa Bwana wetu Yesu kristo, ambao kwa huo ulimwengu umesulibishwa kwangu, na mimi kwa ulimwengu" (Wagalatia 6:14).

Tunaanzia wapi tena? Kama kuna mdhambi hapa, unaanza pale msalabani ambapo unajitambulisha mwenyewe kwamba umekufa pamoja naye. [1]

Inabidi tutambue kwamba tunapaswa kufa ili kuleta maisha mapya. Kwa hiyo amesema mengi katika hili"Kama unataka kuniona mimi, inakupasa au ni lazima ufe, ufe katika utu wako, na hapo sasa utaleta maisha mapya".

Sasa, kama tunataka kumuona yeye, kama unatarajia kuja kumuona Yeye, hutamuona Yeye kwa kujiunga na kanisa, vitabu Fulani vya sheria za kushika, kanuni Fulani zakutumikia. Utamuona Yeye pale unapokufa.
Unapokuja msalabani na umesulibishwa wewe mwenyewe, hapo sasa utaweza kumuona Yesu.

Wale Wayunani walisema katika Yohana mtakatifu 12.20-25
" Tunataka kumuona Yeye". Kwanza, kabla Yesu hajasema kitu chochote, Aliwaelekeza mahali ambapo wangemuona Yeye. Kama watu wote wa mataifa au watu wote, unamuona Yesu pale msalabani ukiwa umesulubishwa pamoja Naye.

Leo tunajaribu kumuona Yeye katika kila kitu. Tunajaribu kumuona katika jengo la kanisa. Tunajaribu kumuona Yeye katika dhehebu. Tunajaribu kumuona yeye kwa kukiri kanuni tunajaribu kumuona Yeye kwa kujaribu kushika siku Fulani Fulani, kwa kutii maungamo Fulani. Lakini hatuwezi kumuona Yeye mpaka tufike Msalabani. Pale tunasulubishwa tunaanguka kwenye mavumbi ya dunia, na tunakufa sisi wenyewe, na halafu kuzaliwa upya tena. Hapo tunampata Yesu.

Oo wengi leo wanajaribu kujishikilia wenyewe na kuwa na mawazo yao. Ninayo njia yangu kwa hilo. Naamini hili, lakini huwezi kumpata Kristo mpaka ufe wewe mwenyewe na umkubali Yeye. Neno, hapa unapata uzima. [ 2 ]

Katika kufikiri kwake Mungu….. Mungu, Yule Roho Mkuu, pale mwanzo kabla hakujawa na mwanzo, Yeye alikuwa Mungu. Na je ulifahamu kwamba ulikuwa ndani yake wakati huo? Kama wewe ni Mkristo ulikuwa ndani yake wakati huo. Na kama ni hivyo, uungu wote uliumbika katika utu (Nafsi) wa Yesu Kristo (Kolosai 2:9-10) na Hapo Yesu alipokuja msalabani, Nilikufa pamoja naye, kwa maana nilikuwa ndani yake wakati huo. (2Tim 2.11-13) kwa maana alikuwa ni udhihirisho wa neno lote, akijua kwamba baadaye tutadhihirishwa. Na tulikuwa msalabani pamoja naye. Tulienda kaburini pamoja naye, na tulifufuka pamoja naye katika kufufuka kwake, Na sasa tumeinuliwa kwa Roho wake pamoja naye kwenye kiti cha Neema, tukiketi pamoja naye katika ulimwengu wa Roho ndani ya Kristo Yesu, siku zote
(Efeso 2:4-6) kwa maana kama vile chembe ya uhai ya asili inavyoendelezwa, inavyorutubishwa kutoka baba na baba kwenda kwa baba na baba, kwenda kwa baba, kadhalika na mbegu ya Kristo inavyorutubishwa. Hivyo ndiyo sababu Mungu hutumia roho ya Eliya mara tano tofauti. Ni nini ni kule (kurithiana ) kuendeleza.

Kama vile tu maisha yako ya asili na uhai na tabia zinavyorithishwa kutoka katika kuzaana kwa asili kutoka kwa baba. Kadhalika Roho wa Mungu ambaye alichaguliwa kimbele kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu (2Tim 1:9-10). Na wakati neno lote la Mungu lilipokamilika lilikusanywa kuwa mwili wa kibinadamu uitwao Yesu Kristo, Pale Mungu alinifanya nilipie dhambi zangu kwa yeye. Ndipo akanifufua pamoja naye katika ufufuo (Rumi 6:4-5). Na sasa tumeketi pamoja naye na nguvu na mamlaka juu ya kila shetani (Waefeso 2:4-7). Oh kama unaweza tu kuamini yale Mungu aliyotupa. Lakini kama hukuketi pamoja naye pale, huwezi kuwa nayo. Na kama umeketi pale, na huamini na unaogopa kutembea, hutaweza kamwe kuitumia. Lakini kama umeketi pale, utaitumia, kwa maana umewekwa kufanya unachofanya (Kolosai 1:-12-15). [3 ]

Na Mungu alipoangalia chini kwenye mwili wa Yesu Kristo….Roho alimuacha yeye pale bustani ya Gesthemane; alipaswa afe kama mwanadamu, (Matayo 26:36-46) kumbukeni marafiki haikuwa lazima afanye hivyo. Hivyo alikuwa Mungu. Mungu akaupaka mafuta ule mwili, ambao ulikuwa mwili wa kibinadamu na haikuwa lazima afanye hivyo….kama ange enda pale kama Mungu, asingeweza kamwe kufa kifo kama hicho; huwezi kumuua Mungu, Haikuwa lazima afanye hivyo; lakini kumbuka, Alienda pale Na wewe ukiwa ndani yake unaona? Mungu bado hajamtenganisha Bibi arusi kutoka kwa Bwana arusi bado kwa hiyo Mungu alipoangalia kwa chini mwili wa Yesu Kristo, aliwaona wote mume na mke. Vyote vilikombolewa katika mwili huo mmoja. Unaona? Wote ni mmoja, wote ni kilekile, Neno lile lile. Neno lilelile lililonenwa juu ya Bwana arusi linanena juu ya Bibi arusi. [4]

Na hivyo ndivyo Mungu alivyo. Sheria mbili tofauti na mojawapo ni sheria ya mauti, na nyingine ni sheria ya uzima. Mungu ana sheria mbili. Kumfuata yeye, na kumtumikia, na kumuabudu yeye ni uzima, kumkataa ni mauti. Ziko sheria mbili ndani ya Mungu.

Sasa, moja ya sheria hizi ilifanywa – ilijulishwa kwa dunia katika mlima Sinai (Kutoka-20). Mungu alitoa sheria kwa Musa na Israel. Siyo kwamba sheria ingaliweza kuwasaidia, lakini sheria ilielekezwa kwao tu wajue kwamba wao ni wenye dhambi (Rum 7:7-17). Mpaka wakati ule hawakujua dhambi ni kitu gani, mpaka walipopata sheria (Rum 5:12-21). Haiwezekani kuwe na sheria bila adhabu. Na sheria siyo sheria bila adhabu. Kwa hiyo sasa kuvunja sheria ni dhambi, na mshahara wa dhambi ni mauti. Kwa hiyo sasa mpaka Mungu alipowapa sheria, kabla ya hapo hawakuwa wanahesabiwa makosa. Kama hakuna sheria hapa inayosema huwezi kuendesha zaidi ya maili ishirini kwa saa, hapo sasa unaweza ukaendesha zaidi ya maili ishirini kwa saa . Lakini kama ipo sheria inayokataza usifanye, hivyo basi ipo sheria na adhabu nyuma yake (Rum 6:23).

Sasa, Sheria ya mauti iliamrishwa pale mlima wa Sinai ambayo ili muambia mtu kuwa yeye ni mwenye dhambi, na kuvunja sheria za Mungu ni mauti (Ezeki.18:20) lakini hakuna wokovu katika sheria. Yenyewe ilikuwa Polisi tu na wakukutupa gerezani, haikuwa na kitu chochote cha kukutoa nacho nje, lakini tena alitoa sheria nyingine. Hiyo ilikuwa pale mlimani pa Kalvari (Yohana 19:17-30) ambapo dhambi ilichukuliwa na Yesu Kristo (Isaya 53:5-6); (2kor. 5:18-19). Na pale ile adhabu (ya dhambi) ililipwa, na siyo na sheria, lakini kwa neema tumeokolewa kwa Neema ya Mungu kwa kutujua kimbele kwa ufahamu wa Mungu wa kimbele wa utu wetu (Efeso2:8-9). [5 ]

Wakati Mchungaji Mkuu alipopigwa, yule kondoo mkubwa Nabii, alipopigwa nyuma pale, alisema"imekwisha" (Yohana 19:25-30). Na dakika hiyo, mara tu baada ya Mchungaji huyu kupigwa, ilikuwa imeisha. Swala la dhambi lililipwa hakukuwa na dhambi tena. Zilikuwa safi ile adhabu ililipwa. Waaminio ambao majina yao yameandikwa katika kitabu cha uzima, wakiwa wamechaguliwa kimbele Tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu, ilikuwa imekwisha dakika ile ambayo Yesu alisema imekwisha (Ufunuo 13:8). [ 6 ]

Na kusudi lote limeachwa ndani ya Yesu Kristo kuwa Mungu mwenyewe, kuchukua adhabu ya sheria yake (mauti) afe amkomboe mkewe aliyepotea kwa kumkataa Yeye. [ 7 ]

Kama umgonjwa , natumaini ningeweza kukuponya, lakini hakuna mtu awezaye kufanya hivyo. Imekwishafanywa hivyo. Uponyaji unao mwenyewe. Ni imani yako katika kazi iliyokwisha ambayo Mungu aliifanya pale msalabani kwa Yesu Kristo (Kolosai 2:13-15). Na nje ya hapo, hakuna uponyaji. Nje ya hapo hakuna wokovu. Hakuna kanisa, hakuna dhehebu, hakuna kanuni, hakuna chochote kinachochukua. Wokovu Yesu Kristo" Yeye aliumizwa kwa maovu yetu; na kwa kupigwa kwake sisi tumeponywa aliumizwa kwa maovu yetu, maovu, yetu kwa kupigwa kwake sisi tuli (unaona ni ya wakati uliopita)- tuliponywa (1Petro 2:24).[8]

Sasa, jambo lile lile ni hili: kama wewe ni mwana wa Mungu, na kama mimi ni mwana au binti wa Mungu, tulikuwa ndani ya Mungu tangu mwanzo. Na wakati Yesu alipokuwa ukamilifu wa Neno hapo tulikuwa ndani yake kama chembe Aliposulubishwa, tulisulubishwa katika mwili wake (Rum 6:6). Alipofufuka kutoka kwa wafu, tulifufuka pamoja naye. Na sasa, tangu tulipolitambua hilo, sasa tumeketi pamoja naye katika ulimwengu wa Roho ndani ya Yesu Kristo. (Efeso 2:4 -7). Sisi kama ni wana na binti za mungu, tu watoto wa mungu. Hivyo basi sisi ni sifa za Mungu. (Wagalatia 4:6). Hapo sasa tunao uzima wa milele. Na Mungu ndiye pekee aliye uzima wa milele uliopo. Hivyo basi tulikuwa ndani yake tangu mwanzo. Na wakati Yesu alipokuwa lile Neno lote, hapo sasa tulikuwa sehemu yake (Yohana 1:1-14). Ameni. Tuko hapo. Hilo linapokuwa pale, hakuna Shetani, hakuna nguvu, hakuna chochote kiwezacho kulisogeza hilo. Huo ni nguzo ya msingi kwa nafsi. [9]

Lakini kitu halisi, kilichoteuliwa na Mungu, chembe ile halisi, Mbegu ile halisi, nafsi ya Mungu iliyokuwa ndani ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu…… kumbuka, ninyi ambao mnae Roho wa Mungu ndani yenu usiku wa leo, mlikuwa pale ndani ya Kristo, kwa sababu alikuwa ukamilifu wa neno. Alikuwa ukamilifu wa Neno kwa jinsi ya mwili (Kolosai 2:9-10). Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu na nafsi yake (2Wakorintho 5:18-19). Unaamini hilo? Angalia, alikuwa ndani ya Kristo. Sasa kama ulikuwa ndani ya Mungu, chembe ndogo, Neno, sifa kutoka mwanzo, hivyo ulitembea pamoja Naye hapa duniani; ulizungumza naye hapa duniani, uliteswa pamoja naye hapa duniani; ulikufa pamoja naye pale Msalabani; na ulifufuka tena pamoja naye; na sasa umeketi pamoja naye katika ulimwengu wa roho ndani ya Kristo Yesu, ulizungumza naye, Neno, kadiri linavyokulisha nafsi yako, kwamba" Mtu ataishi kwa kila Neno litokalo……… (Matayo 4:1-4). [10]

Sasa unaona, kama ulijulikana na Mungu kimbele, sasa unakuwa sehemu ya Mungu. Na njia pekee unayoweza kuwa mwana wa Mungu au binti wa Mungu, lazima uwe sehemu ya Mungu na Mungu hajakamilika bila ya wewe. Lazima iwe hivyo. Hiyo ni sawa, kwa sababu kuna moja, njia pekee ya kupata uzima wa milele, na hiyo ni Mungu na yeye pekee anao uzima wa milele. (Zaburi 36:9). Unaona? Sasa, na ulikuwa sehemu yake na sana sana kuwa ni sifa zake, au ulikuwa katika mawazo yake hapo mwanzo. Na kwa sababu alikufikiri wewe tangu mwanzo, inakupa ule mvuto mdogo wa kumuelekea yeye. Hicho ndicho kinachopaswa kihuishwe wengineo hawataweza kuhuishwa, kwa sababu hawanacho, hivyo ndivyo ilivyo. [11]

Mungu akijua tangu mwanzo yule ambaye ataokolewa na yule ambaye hataokolewa, kwa hiyo alishuka chini na akimfuatia adui kupitia maisha, kupitia kifoni, kupitia paradiso, mpaka kuzimu (Waefeso 4:8:-10) na njia hiyo yote toka utukufuni hadi kuzimu, na akamnyang'anya mamlaka ya kuzimu, na funguo akazichukua kwa shetani, na akafufuka tena, na kuwarudishia wanadamu, kwamba wanaweza kuwa wana na binti wa Mungu tena (Ufunuo 1:17-18).

Yesu alichinjwa tangu lini? Pale msalabani? Hapana Bwana. Yesu alichinjwa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu." Tazama kondoo wa Mungu ambaye alichinjwa kabla ya kuweka misingi ya ulimwengu". (Ufunuo 13:8). Mungu pale mwanzo alipoona dhambi, aliona kile ambacho kimetokea, alilinena Neno na Yesu akachinjwa kabla ya misingi ya ulimwengu. Na kila mtu aliyeokolewa, aliokolewa

(kutokana na Biblia) yule kondoo alipochinjwa katika mawazo ya Mungu kabla ya misingi ya ulimwengu (ufunuo 17:8) ulikuwa imeingizwa katika wokovu hapo. Sasa utafanyaje juu ya hilo? [12]

Ulikuwa ndani yake kama wazo; sasa wewe ni mtu unaweza ukawa na ushirika naye. Unaona? Kama ulivyokuwa ndani ya baba yako hapo mwanzo, lakini sasa ninyi ni wana na binti, kiasi kwamba mnaweza kuwa na ushirika na wazazi, sasa, tu wana na binti wa Mungu, tuwezao kuwa na ushirika na Baba yetu, Mungu. Unaona? Iko nzuri namna hiyo. Hulipendi hilo? Hapo sasa unakuwa kama yeye (Warumi 8:28-30). Na kama tulikuwa ni wana tulikuwa mawazo yake, na tulikuwa katika umbile lake hapo mwanzo.

Na, kumbuka, kama ulikuwa ndani yake hapo mwanzo; na hapo Yesu ambaye ni Mungu, Neno alipofanyika mwili na akakaa kwetu (Yohana 1:1-3,12-18) hapo sasa ulikuwa ndani yake. Ulifufuka ndani yake. Na sasa umeketi pamoja naye katika ulimwengu wa Roho ndani yake (Wakolosai 2:11-15). [13]

Yesu alipoteseka katika ule mwili, Aliteseka……….. kwa sababu mwanaume na mwanamke ni mtu mmoja. Hawa alichukuliwa kutoka kwa Adamu (Mwanzo 2:18-25) na kanisa………..kumetokea nini? Mungu alifungua ubavuni kwa Adamu na akachukua kutoka pale msaidizi, yule Bibi Arusi. Na Mungu alifungua ubavuni mwa Yesu pale msalabani na kumchukua yule Bibi Arusi Unaona? Na Yesu alipokufa pale msalabani…………..

Kumbuka, Bibi Arusi hukuchukuliwa kutoka katika mwili mpaka ulipokuwa umekufa. Alikuwa tayari amekufa na walikuwa wanaenda kuvunja miguu yake. Na nabii alisema, "Hakuna hata mfupa wake utakaovunjwa" sasa walishachukua nyundo wavunje mguu, na mtu akakimbia na mkuki na ukachoma mpaka moyoni mwake, na maji na damu vikatoka; alikuwa tayari amekwisha kufa (Yohana 19:31-37). Alikuwa tayari amekombolewa katika mwili kwa mauti yake. Kwa hiyo hakuna dhiki kuu kwa Bibi Arusi. Unaona? Anaingia ndani. Lakini lile kanisa la Mataifa wale wanaomwamini na kuchukua msimamo wa madhehebu, maungamo na kadhalika….. [14]

Nimejitambulisha naye katika mauti yake. Nilikufa pamoja Naye alipokufa pale msalabani , na nilifufuka tena katika asubuhi ya pasaka pamoja naye katika nguvu za ufufuko wake. Mimi ni shahidi wa hilo. Nilikufa pamoja naye pale Msalabani, nilifufuka naye siku ya pasaka. Halleluya. Kuwa sehemu yake lazima nitambulishwe pamoja naye. Nilitambulishwa naye katika Mauti yake. Nilitambulishwa Naye katika mauti yake. Nilitambulishwa naye katika mateso yake. Nilitambulishwa naye wakati madhehebu yalipomkataa. Nilitambulishwa naye walipomfukuza atoke hekaluni, walipojaribu kumuuwa Yeye. Nilikuwa naye pale. Nilikuwa pamoja naye katika mauti yake, niliinuka pamoja Naye katika ufufuko wake. [15]

Kama nilivyosema usiku ule mwingine, kama mimi ni Mkristo, lazima nitambulishwe na kila tabia ya Biblia. Inabidi nisimame na Noah na kuhubiri pamoja naye katika siku zake na kuwaonya watu. Hiyo ni kweli, inabidi nisimame mlima wa karmeli peke yangu na Eliya. Inabidi nisimame pale msalabani na nisulubishwe kwa nafsi yangu na mawazo yangu, pamoja naye (Wagalatia 2:19-21). Lakini tena nimefufuka pamoja naye katika pasaka, nikiwa mshindi katika mambo yote. Tabia zote za kimwili na tamaa za dunia, nimeinuliwa juu ya hizo kwa njia ya yeye. [16]

Musa alikuwa ndani yake Yoshua alikuwa ndani yake. Na kama uko ndani yake (1Kor12:13) ulikuwa ndani yake kabla ya kuwepo misingi ya ulimwengu, familia ya Mungu; uliteswa pamoja naye; ulikufa pamoja naye; ulienda msalabani pamoja naye; uliinuliwa pamoja naye' na sasa uko pamoja naye; ukiwa umekaa katika ulimwengu wa roho, ukiudhihirisha ujumbe wa wakati kwa ulimwengu, Nuru ya dunia (Matayo 5:14-16). [17]

Nukuu za kiingereza:

*[1] Shalom (64-0112) Aya 197, [2] Mabwana tunataka kumwona Yesu (61-1224) uk15, [3] Mungu wa wakati huu muovu, Ayubu 67-68, [4] kuchomoza kwa jua uk 34 [5] mahali Mungu alipochagua pa kuabudia (65-0220), Aya 21-23 [6] kwa nini ilikuwa ni wachungaji aya 181 [7] Kristo ni siri uk 26. [8] kitendawili (65-0117), Aya 25 [9] Kristo akifunuliwa katika Neno lake mwenyewe, Aya 28 [10] Matukio ya leo yakiwekwa wazi na Unabii Aya 172 [11] usizitegemee akili zako mwenyewe Aya 17 [12] Waebrania sura 7 sehemu ya 1 uk. 298/324 [13] Nguvu ya kugeuzwa, Aya 297 [14] Maswali na majibu (64-0823m) uk, 953 [15] kila kipeo kilicho tambulishwa cha Mungu aya 78 [16] wakati wa mavuno Aya 201 [17] mahali pekee Mungu alipochagua pakuabudia (65-1128M) Aya 271.*

---

Jiwe la kiroho la kujengea na. 143 kutoka Neno lililofunuliwa la saa hii, iliyokusanywa na Gerd Rodewald, Friedenstr. 69, D- 75328 Schomberg Germany, simu (+49) 72357613 Fax – 3306

---

Atakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia. Na kazi ya haraka itaizunguka dunia zile mbegu zitaingizwa katika magazeti na vitu vya kusomea, mpaka kila mbegu ya Mungu iliyochaguliwa kimbele imesikia hilo (Ndg. Branham katika mwenendo utaratibu na mafundisho Uk. 724)

*Kwa nakala zaidi za kiingereza au kiswahili Andika kwa:*

*Charles E. Y. Kanju,*
*Box 553 Korogwe - Tanga*
*E-mail: Chaelika@livel.com*
*Cellphone: 0784 704299/ 0718230098*